


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**

Telegrams "UTUMISHI", DSM.  
Simu: 2118531-4  
Fax: 2125299  
Barua pepe: permsec@utumishi.go.tz



Menejimenti ya Utumishi wa Umma,  
Utumishi House  
8 Barabara ya Kivukoni  
S.L.P. 2483  
11404 Dar es Salaam

*Tafadhali unapojibu taja:*

**Kumb. AC.260/264/01/30**

**04 Februari, 2015**

Makatibu Wakuu wote,  
Makatibu Tawala wa Mikoa wote,  
Wakuu wa Taasisi za Serikali,  
Wakuu wa Idara Zinazojitegemea,  
Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa na Miji wote,  
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri za Wilaya wote,  
**TANZANIA BARA.**

**YAH: WARAKA WA MAENDELEO YA UTUMISHI NA.2 WA MWAKA**  
**2013 KUHUSU MIUNDO YA UTUMISHI YA KADA YA**  
**WATEHAMA CHINI YA WIZARA YA MAWASILIANO,**  
**SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Tafadhali husikeni na somo tajwa hapa juu.

2. Pamoja na barua hii, nawaleteni Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na.2 wa Mwaka 2013 wa Miundo ya Utumishi ya Kada ya WATEHAMA chini ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa ajili ya utekelezaji.

3. Utekelezaji wa Waraka huu utazingatia mambo yafuatayo:-

- a) Kwa watumishi watakaoingia kwenye Miundo ya Utumishi ya Kada za Maafisa TEHAMA na Maafisa TEHAMA Wasaidizi, Mamlaka husika zitapaswa kuwapanga kwa kufuata sifa na majukumu yaliyoanishwa kwa kila fani. Kwa watumishi ambao hawana sifa mojawapo ya zile zilizoainishwa katika Miundo hiyo wabakie katika miundo yao ya zamani (dying cadre) hadi watakapopata sifa.

b) Mahitaji ya utekelezaji wa miundo hii yazingatiwe wakati wa kuandaa Ikama na Bajeti ya mishahara kwa mwaka wa fedha 2015/16.

c) Waajiri wote kuhakikisha maelekezo ya Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa mwaka 2009 kuhusu Udhubiti wa Ongezeko la Madeni ya Serikali kwa Watumishi wa Umma yanazingatiwa wakati wa utekelezaji wa miundo hii.

4. Kutokana na maelezo yaliyomo katika Aya ya 3 ya barua hii, ni muhimu waajiri kuhakikisha kuwa wakati wa utoaji wa barua za kubadilishwa/ kuajiriwa kwa watumishi katika miundo hii tarehe za kuanza mabadiliko hayo zisisababishe kuwepo kwa malimbikizo ya mishahara.

5. Nawashukuru kwa ushirikiano wenu.



HAB Mkwizu

**KAIMU KATIBU MKUU (UTUMISHI)**